فضل السحور

اللغة السواحلية

كتبه فضيلة الشيخ العلامة : صالح بن فوزان الفوزان.

ترجمه: الشيخ: ياسين طه حسن .

مراجعه: يونس كنون

FADHILA ZA KULA DAKU

Kiswahili.

Imeandikwa na: Imaam Swaalih bin Fawzan Al-Fawzaan.

Imetafsiriwa na: Yasini Twaha Hassani

Imepitiwa na: Yunus Kanuni Ngenda

بسم الله الرحمن الرحيم

Utangulizi

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, na rehma na amani zimwendee Mtume wetu Muhammad (s.a.w) na watu wake na Maswahaba wake wote. Amma baad:

Mtu ni mwenye haja ya kula na kunywa. Kwa ajili hii Allaah Hakumkataza mfungaji kula, kunywa na kufanya jimaa wakati wa usiku isipokuwa tu wakati wa mchana, kuanzia pale ambapo alfajiri inapoingia mpaka wakati jua linapozama. Allaah Anapenda watu wale daku. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema kuhusu daku:

“Kuleni daku. Hakika katika kula daku kuna baraka”.

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Allaah (´Azza wa Jalla) na Malaika Wake wanawaswalia wenye kula daku.”

(Ibn Hibbaan (3467),

Atw-Twabaraaniy i ”

Al-Awsatw” (6434) na

Abu Nu´aym (8/320). Hasan kwa mujibu wa al-Albaaniy katika ”Swahiyh-ut-Targhiyb” (1070).

Kwa nini daku?

Daku si ni chakula tu ambacho mtu anakula kwa matamanio?.

Kwa sababu nia yake ni kutekeleza maamrisho ya Allaah ambayo ni kufunga, ili aweze kupata nguvu za kumuabudu Allaah. Kwa ajili hio kila ambavyo daku itacheleweshwa ndio bora zaidi:

وَكُلُوا وَاشْرَبُوا حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ الْخَيْطُ الْأَبْيَضُ مِنَ الْخَيْطِ الْأَسْوَدِ مِنَ الْفَجْرِ

”Na kuleni na kunyweni mpaka ibainike kwenu weupe (wa Afajiri) kutokana na weusi (wa usiku).” (02:187)

Ama yule anayekula usiku mzima na kujaza tumbo lake kisha analala nyuma na wala haamki kula daku pamoja na Waislamu wenzake na wala haswali hata al-Fajr, huyu kwa hakika hakutekeleza maamrisho ya Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala).

Amechofanya ni kutekeleza maamrisho na hawaa ya nafsi yake. Yuko macho usiku mzima ambapo anakesha kwa kumuasi Allaah na analala wakati ambapo anatakiwa kumtii Allaah (´Azza wa Jalla).

CHANZO:

http://www.alfawzan.af.org.sa/node/%205824